

NAFASI ZA KAZI

Shirika la SOS Children's Villages Tanzania ni shirika lisilo la kiserikali ambalo limejikita katika kuhudumia watoto waliopoteza malezi au wale walio katika hatari ya kupoteza malezi ya wazazi. Shirika limejikita katika kutoa malezi mbadala kwa watoto kwa kuwapatia familia mbadala katika makao na ndani ya jamii. Shirika la SOS Children's Villages Tanzania limekuwa likifanya kazi nchini Tanzania tangu mwaka 1991. Shirika limekuwa likitoa huduma ya malezi mbadala, kuimarisha familia na elimu kwa watoto katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Mwanza, Iringa, Mufindi, Unguja na Pemba. Shirika la SOS Children's Villages Tanzania linatafuta mtu mwenye sifa zifuatavyo kujaza nafasi ya:

Nafasi Ya Kazi: Mama Msaidizi wa SOS Children's Villages (Nafasi tatu 3)

Kituo cha Kazi: Arusha

Anaripoti Kwa : Mratibu wa Malezi Mbadala

Dhumuni ya kazi

Mama Msaidizi analo jukumu la kuzungukia nyumba za malezi za SOS, kufanya kazi za akina Mama wakiwa likizo na kutoa msaada unaohitajika kwa walezi wakuu pale inapobidi. Mama Msaidizi hufanya kazi kwa kushirikiana na Mama ili kuhakikisha wanatoa huduma za uhakika za kimalezi kwa watoto walio chini ya uangalizi wao. Mama Msaidizi ni sehemu muhimu katika familia za SOS; hivyo hana budi kuwa mtu anayejali, muelewa, mkomavu na mwajibikaji ili aweze kuaminika na watoto kama mlezi wa kweli.

Majukumu ya kazi ya Mama Msaidizi.

- Anamsaidia Mama Kwa kufanya kazi kwa karibu na Mama na Kuhakikisha kuna Ustawi mionganoni mwa Watoto wanaowalea.
- Anabeba majukumu ya Mama wakati hayupo, anaishi kwenye nyumba za SOS na kufanya kazi zote anazopaswa kufanya Mama, majukumu haya ni pamoja na kufua na kunyosha nguo za watoto, kupika, kuwaogesha na usafi wa jumla wa nyumba.
- Anamsaidia Mama katika kusimamia maendeleo ya kielimu ya watoto, mfano kuwasimamia watoto wakati wakisoma, kuwasaidia watoto kufanya kazi wanazopewa na walimu.
- Anaelewa na kusimamia haki na wajibu wa kila mtoto.
- Anamsaidia Mama kupanga na kusimamia shughuli za burudani, michezo au kufanya ziara za nje ili kujenga umoja na mshikamano.
- Anatoa taarifa sahihi kwa mama juu ya jambo lolote ambalo limejitokeza kwa mtoto lisilo la kawaida kwa hatua zaidi.
- Anamsaidia Mama kufanya kazi kama kupanga bajeti, ununuzi wa bidhaa, upangaji wa mlo na utoaji wa hesabu za fedha kama inavyotakiwa.
- Anawaongoza Watoto ili waweze Kujitegemea, anashauri watoto kuijendeleza kielimu na kimafunzo ili kuwawezesha kukabiliana na maisha baada ya kuondoka kwenye Kijiji cha Malezi cha SOS.

Sifa za Muombaji

- Awe na elimu si chini ya Sekondari, Cheti cha mafunzo cha Malezi ,Makuzi na Maendeleo ya awali ya Mtoto (ECD) ni sifa ya ziada
- Awe hana majukumu makubwa ya kifamilia, asiwe na watoto wenyе umri chini ya miaka 12
- Awe yuko tayari kuishi katika Kijiji cha SOS kama mama wa watoto wanaohitaji malezi.
- Uwezo wa kuongea kwa lugha ya Kiingereza ni sifa ya ziada.
- Kama hana cheti cha sekondari awe na cheti chochote cha malezi ya watoto au barua yoyote ambayo inamthibitisha kuwa amekuwa akijihusisha na malezi ya watototo wanaofanana na hawa.
- Mama aliyaliza kidato cha nne atapatiwa kipaumbele.

Ili kuomba nafasi hii, tuma barua yako ya maombi ikieleza uzoefu na sifa na uwezo ulio nao ikiiambatanishwa na vivuli vya vyeti, Wasifu (CV), na majina ya wadhamini watatu (Referees) kwa anuan;

The National Director ,SOS Children's Villages Tanzania.

P.O Box 80462 Dar es Salaam, Tanzania

au kwenye email;

recruit.sostanzania@sos-tanzania.org

216803001

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 22. 04.2022.Ofisi itawajulisha wale ambao watakao chaguliwa kwenye usahili tu.